MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA TATU - TAREHE 31 JANUARI, 2002

Kikao kitaanza saa Tatu Asubuhi
na Dua Zitasomwa

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):

Taarifa ya Utendaji na Hesabu za Mwaka za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2001 (The Annual Report and Accounts of the Presidential Parastatal Sector Reform Commission for the Year ended 30th June, 2001)

II. MASWALI

OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):

16. MHESHIMIWA PROF. MWAKYUSA (RUNGWE MAGHARIBI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa): Kwa kuwa hospitali ya Wilaya ya Rungwe- Mjini Tukuyu kwa muda mrefu imekuwa na daktari mmoja tu ambaye licha ya kuhudumia wagonjwa, hufanya kazi za utawala kwenye hospitali hiyo pamoja na vituo vinne (4) vya afya na Zahanati hamsini (50); na kwa kuwa Serikali hupata madaktari wapya wasio chini ya hamsini (50) kila mwaka;

    Je, Serikali inaweza kuweka kipaumbele kwa wananchi wa Rungwe cha kuwapatia angalau madaktari wawili (2) kwenye mgao ujao wa madaktari kwa lengo la kunusuru maisha ya wananchi husika na kuondoa usumbufu mkubwa walio nao sasa.

17. MHESHIMIWA BWANA (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa): Kwa kuwa Tume ya Jiji la Dar es Salaam ilifikia kiwango cha ukusanyaji wa Mapato kwa zaidi ya Shilingi bilioni nane (8 bil./-) kwa mwaka 1998 ikilinganishwa na Shilingi milioni 900 (900m./-) kwa mwaka, kabla ya Tume ya Jiji kuundwa:-

(a) Je, tangu kuundwa kwa Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, mwenendo wa ukusanyaji wa Mapato katika kipindi cha Januari-Disemba, 2000 sasa ukoje;

(b) Kuna mafanikio gani na mapungufu yapi.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS:

18. MHESHIMIWA MWANANZILA (KALAMBO): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais: Kwa kuwa Serikali imekuwa ikihimiza wananchi wahifadhi mazingira kwa kupanda miti ya aina mbalimbali:-

(a) Kwa kuwa , Serikali inajua wazi uharibifu wa mazingira unatokana na sababu kama ufugaji usio na mpangilio, uchomaji moto misitu na ukataji wa miti hovyo; Je, Sera yake ina dosari zipi zinazosababisha uharibifu wa mazingira uendelee nchini kote licha ya kukemea uharibifu huo unaotokea;

(b) Kama Serikali imetenga maeneo ya hifadhi za misitu kwa makusudi, Je, isingekuwa busara kwa Serikali kutumia Sera zake kuzuia ufugaji wa kuhamahama kiholela ili usiendelee kote nchini kama ilivyotokea hivi karibuni kwenye baadhi ya maeneo nchini, na kwamba kama hatua hiyo haitachukuliwa baada ya miaka 20 au 30 nchi yetu nzima itakuwa katika sura ya aina moja ya nusu jangwa kama ilivyo kwa Mikoa ya Kati;

(c) Je, Serikali haioni kwamba kwa kutozuia uhamaji holela wa mifugo toka Mkoa mmoja na kuingia Mkoa mwingine, kunaonyesha upendeleo wa matumizi ya mazingira kwa wachache na kuwaharibia wale walioyalinda kwa karne nyingi, na hivyo Serikali ilaumiwe kwa kusaidia kuharibu mazingira kutokana na sera zake mbaya.

19. MHESHIMIWA MWENDA (KILWA KUSINI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais: Kwa kuwa Kilwa inayo historia nzuri ya utunzaji wa mazingira na ukweli huo unadhihirika kwa kuwa na Ukuta mkubwa uliojengwa kuzunguka bahari ili kuzuia mmomonyoko unaoweza kusababishwa na mawimbi ya maji; na kwa kuwa ukuta huo uko kwenye hatari ya kutoweka:-

(a) Je, ni lini Serikali itatembelea eneo hilo ili kuona hali halisi ya ukuta huo;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuukarabati ukuta huo ambao pia ni wa kihistoria kabla haujatoweka kabisa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

20. MHESHIMIWA MISSANGA (SINGIDA KUSINI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi: Kwa kuwa utaratibu wa kuajiri Askari Polisi ni wa aina mbili, yaani askari wanaoajiriwa kwa masharti ya pensheni na wale wanaoajiriwa kwa masharti ya mkataba/bakshishi, jambo ambalo limezua malalamiko mengi hasa kwa askari ambao wameajiriwa kwenye mkataba/bakshishi na kwamba wamevunjika moyo kwa sababu mara mkataba unapomalizika hupata maslahi duni ikilinganishwa na wale wa masharti ya pensheni;

Je, Serikali haioni kwamba ni busara kuwa na utaratibu wa aina moja wa ajira kwa msingi wa pensheni kwa

askari wote ili kudumisha usawa, umoja na mshikamano katika Jeshi hilo.

WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:

21. MHESHIMIWA AZIZA SLEYUM ALI (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi: Kwa kuwa kazi ya kuthibitisha ramani za viwanja (site plans) kote nchini hufanywa na Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi; na kwa kuwa tatizo la ukubwa wa nchi na uzito wa kazi hiyo husababisha mlundikano wa maombi na ucheleweshaji wa kazi hiyo:

    Ili kupunguza tatizo hilo, Je, kwa nini Serikali isikasimu madaraka ya kuifanya kazi hiyo kwa Mikoa au Kanda.

WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:

22. MHESHIMIWA ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH (KILOSA): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko: Kwa kuwa ni muhimu kuendeleza mipango ya masoko kwa ajili ya mazao yetu na bidhaa zetu tunazouza katika masoko ya ndani na masoko ya nje ya nchi yetu na kwa kuwa kila zao na kila bidhaa ina muda wake wa kutumika (life cycle).

    (a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili kwamba mazao yetu na bidhaa zetu tunazouza katika masoko ya ndani na masoko ya nje yapo katika hatua zipi za "Life Cycle".

    (b) Je, Serikali inatumia mikakati gani ya udhibiti wa utafiti na hatua za kuendeleza ubora wa bidhaa na uzalishaji katika kila hatua ya "Life Cycle" ya mazao, bidhaa zetu na masoko ili kukabiliana na ushindani ipasavyo na hivyo kujizatiti katika masoko asilia na kujipenyeza zaidi katika masoko mapya katika hali endelevu.

23. MHESHIMIWA LAIZER (LONGIDO): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko: Kwa kuwa biashara ya mazao ni ya Soko huria lakini bado wakulima wanahangaika kutafuta maeneo ya kuuzia mazao yao na wakati mwingine hutafuta masoko mipakani mwa nchi jirani:-

(a) Je, kwa nini Serikali inawawekea vizuizi ambavyo vinasababisha rushwa;

(b) Kwa kuwa hakuna kampuni za uhakika za kununua mazao ya wananchi; Je, kwa nini Serikali isiwaruhusu wananchi kuuza mazao yao popote hata nchi jirani.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

24. MHESHIMIWA DR. ZAINAB GAMA (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa: Kwa kuwa tarehe 11 Septemba, 2001, lilitokea tukio la Kigaidi huko Marekani:-

(a) Je, ni Watanzania wangapi waliathirika katika tukio hilo;

(b) Endapo kuna Watanzania walioathirika; Je, ni utaratibu gani ambao Serikali iliutumia kuwaarifu Watanzania juu ya hilo.

25. MHESHIMIWA ZAHOR JUMA KHAMIS (CHUMBUNI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa: Kwa kuwa imetajwa katika Mkataba wa Ushirikiano wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa, Ushirikiano huo pamoja na mambo mengine utahusu pia eneo la mambo ya kiuchumi; na kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la uvushaji wa karafuu kwa njia za magendo kutoka visiwa vya Zanzibar kwenda Kenya; na kwa kuwa pamoja na kuwepo kwa

biashara hiyo haramu Serikali ya Kenya haiwakamati wala kuwakemea waendesha biashara hiyo haramu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa hatua ya Kenya ya kutozuia biashara hiyo haramu kutadhoofisha Uchumi wa Zanzibar na pia kuondoa dhana nzima ya Ushirikiano wa dhati wa Masuala ya Kiuchumi kwa nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na hali hiyo.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

26. MHESHIMIWA SHIBILITI (MISUNGWI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara: Kwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara ni mmoja wa wapangaji ndani ya Jengo la Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC); na kwa kuwa kumbukumbu za Shirikisho hilo zinaonyesha kuwa Wizara hiyo ni kati ya wadaiwa wakubwa na yenye matatizo ya kulipia pango.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo;

(b) Je, Wizara inadaiwa deni la kiasi gani; na

(c) Je, ina mpango gani wa kulipa deni hilo.

27. MHESHIMIWA DR. LUOGA (MBINGA MAGHARIBI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara: Kwa kuwa wapo wenye viwanda, na wafanyabiashara binafsi wakiwemo wa mazao ya kilimo wanaokubaliana bei kwa bidhaa/huduma wanazotoa au kununua bila kujali kuwa bei inatakiwa ipangwe na soko; na kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kukiuka Sheria ya "Fair Trade Practices"

(a) Je, kwa kujipangia bei badala ya bei inayopangwa na soko si ukiukwaji wa sheria hiyo;

(b) Je, Sheria ya "Fair Trade Practices" katika mazingira hayo si inawalinda wale wenye uwezo na siyo wanyonge; na kama hivyo ndivyo, isingefaa sheria hiyo ifutwe kwa kuwa utekelezaji wake ni wa upendeleo;

(c) Je, ni kesi ngapi zimeshapelekwa Mahakamani kutokana na ukiukwaji wa sheria hiyo.

WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:

28. MHESHIMIWA NKUMBA (SIKONGE): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo: Kwa kuwa wananchi wa kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda wengi wao hawajauona Mwenge wa Uhuru kutokana na kuwa pembezoni mwa njia zinazotumiwa kwa ajili ya mbio za Mwenge huo kila mwaka; na kwa kuwa wananchi hao kila mwaka hutoa michango ya mafuta ya Mwenge kwa ajili ya Mwenge wasiouona tangu nchi yetu ipate uhuru:-

(a) Je, Serikali iko tayari kurekebisha utaratibu wa njia zinazotumika kwa ajili ya mbio za Mwenge ili wananchi hawa waweze kupata fursa ya kuuona Mwenge wa Uhuru wanaouchangia kila mwaka pasipo kuuona;

(b) Je, ni kwa nini waandaaji wa njia zinazotumika kwa ajili ya mbio za Mwenge wa Uhuru hawajaliona tatizo hilo tangu uhuru la kuwanyima haki watu wa maeneo kadhaa hapa nchini ya kuupokea, kuuona na kuushangilia Mwenge.

29. MHESHIMIWA MHAGAMA (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo: Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto yatima kutokana na ugonjwa hatari wa UKIMWI:

(a) Je, Serikali imejiandaaje katika kuanzisha Vituo vya kulelea watoto yatima hasa wale walio chini ya

miaka mitano (5) hususan katika Mikoa iliyoathirika sana mfano Ruvuma na mingineyo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ruzuku katika vituo vya kulelea watoto yatima vilivyopo kwa sasa ambavyo vinaendeshwa na Mashirika ya Kidini na watu binafsi ili kuwatia moyo.

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza huduma ya malezi na elimu kwa watoto hao mara wamalizapo muda wao wa kuishi katika vituo hivyo.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Mahakama za Kushughulikia Migogoro ya Ardhi wa Mwaka 2002 (The Courts (Land Disputes Settlements) Bill, 2002).

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kumbukumbu na Nyaraka wa Mwaka 2002 *(The Records and Archives Management Bill, 2002).*

DODOMA **K.M.M.**
31 JANUARI, 2002 **KATIBU WA BUNGE**